



**MUUNDO NA MAJUKUMU
YA KAMATI
ZA WANAWAKE RAAWU**

1.0 UTANGULIZI

Kuanzishwa kwa Kamati za Wanawake katika Chama cha RAAWU ni mojawapo ya mkakati wa kuhakikisha kuwa wanachama wanawake wanashiriki kikamilifu katika shughuli za chama na hususan katika suala zima la uongozi, kwani kwa jumla idadi ya wanawake viongozi ni chini ya theluthi moja.

2.0 MADHUMUNI YA KAMATI ZA WANAWAKE

2.1 Dhumuni kuu

Kuhakikisha wanawake wanaingia katika Muundo wa Chama "*Gender Mainstreaming*".

2.2 Madhumuni mengine

- (i) Kuboresha viwango vya Elimu na Uchumi.
- (ii) Kuingiza wanawake wengi zaidi ili kuimarisha nguvu za Chama.
- (iii) Kuongeza hamasa ya wanawake kushiriki katika shughuli za Chama kama vile kuwakilisha au kuwakilishwa katika vikao mbalimbali.
- (iv) Kuzijua haki na wajibu wa mwanamke mfanyakazi.
- (v) Kupata utetezi wa nyanyaso toka kwa mwajiri na wafanyakazi wengine.

3.0 MUUNDO WA KAMATI ZA WANAWAKE

Kamati za Wanawake zina Muundo ule ule wa Chama. Ngazi ya chini kabisa ni Tawi, ikifuatiwa na Kanda hadi Taifa.

3.1 Ngazi ya Tawi

- (i) Kamati ya Wanawake inaundwa kutokana na wanachama waliopo katika Tawi hilo.
- (ii) Kamati ya wanawake katika ngazi ya Tawi itachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Tawi

- (iii) Kamati inaundwa na watu watano (5) tu kwa kuzingatia uwakilishi wa sehemu za kazi, yaani Mwenyekiti, Katibu, Mweka Hazina na wajumbe wawili.
- (iv) Kamati ya Wanawake ni mojawapo ya Kamati ya Tawi, hivyo itawajibika kama Kamati nyingine kwa Kamati ya Tawi,
- (v) Mwenyekiti na Katibu wa Kamati ya Wanawake atakuwa ni mjumbe wa Kamati ya Tawi, vivyo hivyo Katibu wa Tawi atahudhuria vikao vyote vya Kamati ya Wanawake.
- (vi) **Vikao:** Vikao vya Kamati ya Wanawake vinatakiwa vifanyike kabla ya vikao vya Halmashauri ya Tawi.

3.2 Ngazi ya Kanda

Kamati ya Wanawake katika ngazi ya Kanda itachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Kanda.

- (i) Kamati ya Kanda itakuwa na wawakilishi watano ambao ni:-
 - a. Mwenyekiti
 - b. Katibu
 - c. Mtunza Hazina, na
 - d. Wajumbe wawili.
- (ii) Uchaguzi wa Kamati ya Kanda unazingatia uwakilishi wa Mikoa inayounda Kanda hiyo.
 - (a) Mwenyekiti na Katibu wa Kamati ya Wanawake ya Kanda ni wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Kanda.
 - (b) Katibu wa Chama wa Kanda atahudhuria vikao vyote vya Kamati ya Wanawake vya Kanda.
- (iii) Vikao
Vikao vya Kamati ya Wanawake vya Kanda

vinatakiwa vifanyike kabla ya vikao vya Kamati ya Utendaji Kanda.

3.3 Ngazi ya Taifa

Kamati ya Wanawake ya Taifa itakuwa na wajumbe wafuatao kwa kuzingatia uwakilishi wa Kanda. Kamati hii itakuwa na wawakilishi wafuatao:-

- Mwenyekiti
 - Mweka Hazina na
 - Mjumbe mmoja mmoja kutoka kila Kanda.
- (i) Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake ya Taifa atakuwa mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Chama na Baraza Kuu la Chama.
 - (ii) Katibu Mkuu atahudhuria vikao vyote vya Kamati ya Wanawake ya Taifa.
 - (iii) **Vikao:** Vikao cya Kamati ya Wanawake ya Taifa vinatakiwa vifanyike kabla ya vikao vya Kamati ya Utendaji na Baraza Kuu.

4.0 KAZI ZA KAMATI YA WANAWAKE

4.1 Ngazi ya Tawi

Kamati ya Wanawake katika ngazi ya Tawi itafanya kazi zifuatazo:-

- (i) Itawahamasisha wanawake mahali pa kazi ili waelewe umuhimu wa Chama cha Wafanyakazi na hatimaye kujiunga na Chama.
- (ii) Itatoa ushauri na mapendekezo kwa Halmashauri ya Tawi juu ya masuala yote yanayohusu wafanyakazi wanawake mahala pa kazi.
- (iii) Itahakikisha kuwa Mkataba ya Hali Bora za Kazi inayofungwa mahali pa kazi inajumuisha na kuzingatia masuala ya msingi yanayohusu haki na maslahi ya wafanyakazi wanawake.

- (iv) Itawaelimisha na kuwahasisha wafanyakazi wanawake katika masuala ya Kiuchumi yatakayoweza kuwaongezea kipato katika maisha ili kuondokana na umaskini.
- (v) Itawaelimisha na kuwahasisha wafanyakazi katika masuala ya jinsia na utamaduni na kuwawezesha kupata elimu ya Vyama vya Wafanyakazi.
- (vi) Itawahamasisha na kuwaelimisha wafanyakazi wanawake ili waondokane na fikra za unyonge na kutojiamini na wajione wao ni sehemu ya Taifa na wanayo haki ya kushiriki katika uongozi na shughuli zote za maendeleo, katika jamii.

4.2 Ngazi ya Kanda

Kamati ya Wanawake katika ngazi ya Kanda pamoja na kazi zilizoainishwa katika Tawi itafanya kazi zifuatazo:-

- (i) Itapokea na kujadili hoja na mapendekezo toka matawini na kuyafanyia kazi kwa mujibu wa taratibu na sheria zilizopo.
- (ii) Itabuni na kuweka mipango madhubuti itakayosaidia katika harakati za ukombozi wa wafanyakazi wanawake katika Kanda.
- (iii) Itashauriana na Chama na Taasisi nyingine za maendeleo nchini kuhusu masuala yote yanayolenga katika kuwaendeleza na kuwasaidia wafanyakazi wanawake katika Kanda.

4.3 Kamati ya Wanawake Taifa

Pamoja na kushamirisha majukumu ya Kamati za Wanawake za Matawi na Kanda, Kamati ya Wanawake Taifa itafanya kazi zifuatazo:-

- (i) Itapokea na kujadili mapendekezo ya masuala ya wanawake kutoka katika ngazi za chini

za Chama na kufanyia kazi kwa mujibu wa taratibu, kanuni na sheria zilizopo.

- (ii) Itaandaa mipango ya kuhamasisha wafanyakazi wanawake Kitaifa katika kuelewa umuhimu wa Vyama vya Wafanyakazi na ushirikishwaji katika uongozi wa Chama, Serikalini na katika jamii kwa ujumla.
- (iii) Itashauri Chama katika kubuni sera na mikakati ya kuwaendeleza na kuwasaidia wafanyakazi wanawake.

5. HITIMISHO

Wito unatolewa kwa viongozi wote wa Kamati za Wanawake waliochaguliwa katika awamu ya nne ya uongozi wa RAAWU, kuzingatia maelekezo yaliyotolewa katika Katiba ya RAAWU toleo la mwaka 2009 na maelezo ya kipeperushi hiki, katika kutekeleza majukumu yao ya siku kwa siku ili kukidhi matakwa ya wanachama waliowaweka madarakani. Kwa maelekezo zaidi wasiliana na ofisi yako kwa anuani ifuatayo:-

RAAWU Makao Makuu
S.L.P. 22532

DAR ES SALAAM

Simu za ofisi : 21223762
(VODA) 0767 – 123 762

(AIRTEL) 0786 – 123 762

(TIGO) 0716 – 123 762

Simu za mkononi

0754 – 307728 (Bibi A. Mgaya – Katibu Mkuu)

0715 – 471653 (A. Ndomba Mwinuka-KMEW)